

## HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# eGA: TEHAMA italeta ufanisi utendaji serikalini

Na Romana Mallya

MKURUGENZI Mkuu wa Mam-laka ya Serikali Mtandao (e-GA), Benedict Ndomba, amesema wa-taendelea kusimamia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Ma-wasiliano (TEHAMA) serikalini ili kuleta tija na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Ndomba ameemeleza hayo baada ya hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan kueleza kuwa viongozi wa umma wanapaswa kufahamu na kutumia mifumo mbalimbali ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TE-HAMA) iliyoko serikalini katika

utekelezaji wa majukumu yao. Rais Samia aliagiza viongozi hao kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Mawasiliano wa e-Mrejesho ili kupokea maoni ya wananchi kuhusu serikali na kutoa mrejesho kwa wananchi kupitia mfumo huo.

Akizungumza kuhusu matumi-zi ya mifumo ya TEHAMA serikalini, Mkurugenzi Mkuu Ndomba alisema e-GA itaendelea kusimamia matumizi ya TEHAMA serikalini ili kurahisisha upatikanaji huduma bora kwa wananchi kwa wakati mahali walipo.

"Moja ya maeneo ambayo Rais Samia amekuwa akiyapa kip-

aumbele ni kuimarisha Serikali Mtandao kwa kuhakikisha taasisi za umma zinatumia TEHAMA kwenye utendaji kazi wake na wananchi wanapata huduma za serikali kidijitali mahali popote na muda wote.

"Katika kuhakikisha tunafikia lengo la Rais, e-GA kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma tumetengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA ambayo imesaidia kupunguza gharama, kuokoa muda, kuongeza ufanisi na kurahisishia wananchi kupa-huduma kidijitali mahali walipo," alisema.

Ndomba alisema mifumo wa e-

Mrejesho unawezesha wananchi kutuma kero au malalamiko, maoni, maswali na pongezi kidijitali kwenda katika taasisi yoyote ya umma na kisha kupata mrejesho wa utekelezaji wake kidijitali mahali walipo.

Pia alisema unasaidia kuokoa muda na fedha, kwani mwana-nanchi halazimiki tena kusafiri umbali mrefu kwenda katika ofisi ya umma kwa ajili ya kuwasili-sha malalamiko yake au kufua-tilia utekelezaji wake na badala yake, anaweza kufanya hivyo kidijitali kupitia simu yake ya kiganjani mahali alipo.

Zamani ilikuwa mtu akihi-

taji kutoa maoni au malalamiko kuhusu huduma inayotolewa na taasisi ya umma ilimlazimu kufika katika taasisi hiyo na kuwasili-sha malalamiko yake kwenye sanduku la maoni au kuwasilisha barua katika taasisi hiyo na kisha kufanya ufuatiliaji utekelezaji wake, lakini kwa sasa anaweza kuwasilisha maoni hayo kidijitali," alifafanua Ndomba.

Akiwaapisha wateule wake hivi karibuni, Rais Samia ali-wataka kutumia mifumo wa e-Mrejesho kupokea maoni ya wananchi na kutoa mrejesho kwa wananchi pamoja na serikali kuhusu utekelezaji maoni hayo.